TANGAZO LA SERIKALI NA. 201 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA YA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 722 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 4 kwa kuongeza maneno "kwa maandishi" mara baada ya neno "hayo" lililopo mwishoni mwa kanuni ndogo ya (4).

Marekebisho ya Jedwali la Pili

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Pili kwa-
   (a) kufuta herufi "B." iliyopo chini ya Sehemu A yenye kichwa cha habari "USHURU WA MADINI YA UJENZI"; na
   (b) kufuta herufi "C" yenye kichwa cha habari "ADA YA UKAGUZI NA UMILIKI WA ENEO LA KUCHIMBA MADINI YA UJENZI" na badala yake kuweka herufi "B".

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*